JARIDA MAALUM LA OFISI YA

# WAZIRI MKUU

JARIDA HILI HALIUZWI | TOLEO LA 1 | DESEMBA 2025 | WWW.PMO.GO.TZ




**Ndani**

## DKT MWIGULU: VIONGOZI WA DINI ENDELEENI KUTOA ELIMU YA UMOJA NA AMANI.

WAZIRI MKUU Dkt. Mwigulu Nchemba ametoa wito kwa viongozi wa dini kuendelea kushirikiana na Serikali katika kutoa elimu ya umoja na amani, kupinga chuki...........

## DKT. MWIGULU AAGIZA KUFUTWA KAZI WATENDAJI WA TEMESA.

WAZIRI MKUU Dkt. Dkt. Mwigulu Nchemba ameagiza kufutwa kazi na kufikishwa katika vyombo vya sheria kwa aliyekuwa Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Ufundi na Umeme Tanzania (TEMESA)...........



**DKT. MWIGULU LAMECK NCHEMBA**

**WAZIRI MKUU WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, akimuapisha Dkt. Mwigulu Nchemba kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Chamwino Ikulu jijini Dodoma Novemba 14, 2025.











# KAZI, UWAJIBIKAJI, UADILIFU NA NIDHAMU SERIKALINI

Tangu alipoteuliwa kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba ameonesha kwa vitendo dhamira thabiti ya kusimamia shughuli za Serikali kwa uwajibikaji, nidhamu na kasi inayolenga matokeo.

Uongozi wake umejikita katika kuhakikisha sera, mipango na maamuzi ya Serikali yanatekelezwa kwa ufanisi, kwa wakati na kwa maslahi mapana ya Watanzania.

Katika mapambano dhidi ya rushwa, Waziri Mkuu amekuwa mstari wa mbele kukemea vitendo vinavyohujumu maadili ya utumishi wa umma. Ameweka msisitizo kwa viongozi na watendaji wote kuzingatia sheria, kanuni na taratibu, akisisitiza kuwa rushwa ni adui wa maendeleo na haina nafasi katika Serikali inayowajibika. Kauli na hatua zake zimeimarisha imani ya wananchi kuwa Serikali iko makini katika kulinda rasilimali za umma.

Waziri Mkuu Dkt. Mwigulu aliteuliwa katika kipindi ambacho nchi ilikuwa ikikabiliwa na sintofahamu iliyochochewa na baadhi ya watu waliokuwa wakijaribu kuwachonganisha wananchi na Serikali yao. Kwa ujasiri na uwazi, alisimama mbele ya umma na kueleza ukweli, akiwahimiza wananchi kujitenga na watu wasioitakia mema nchi.

Aliwahimiza Watanzania kulinda miundombinu ya umma na mali za watu binafsi, akisisitiza kuwa uharibifu hauwezi kuwa suluhisho la changamoto za kijamii au kisiasa.

Katika kulinda haki za wanyonge, Waziri Mkuu ameonesha moyo wa usikivu na utetezi wa dhati. Mfano halisi ni pale alipoingilia kati na kuwezesha kijana mjasiriamali wa Dodoma kupata haki yake baada ya kudhulumiwa, hatua iliyotuma ujumbe mzito kwamba Serikali haitavumilia matumizi mabaya ya madaraka dhidi ya wananchi wa kawaida. Msisitizo wake ni kwamba haki haipaswi kuangaliwa kwa hadhi ya mtu, bali kwa misingi ya sheria na utu.

Katika kipindi chake tangu alipoanza kazi, amesisitiza ubora katika utekelezaji wa miradi na nidhamu ya muda, akitaka kila aliyepewa dhamana na kulipwa kwa fedha za Watanzania afanye kazi kwa uadilifu na viwango vya juu.

Kwa mtazamo wake mpana na hamu ya dhati ya kuona Tanzania inaheshimika ndani na nje ya nchi, Waziri Mkuu Dkt. Nchemba anaendelea kuwa nguzo muhimu ya uongozi wa Serikali.

Ni dhahiri kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan, alifanya uchaguzi sahihi kwa kumteua Waziri Mkuu mwenye sifa za kuisimamia Serikali kwa weledi na uthabiti.



# DKT MWIGULU: VIONGOZI WA DINI ENDELEENI KUTOA ELIMU YA UMOJA

**WAZIRI MKUU,** Dkt. Mwigulu Nchemba ametoa wito kwa viongozi wa dini kuendelea kushirikiana na Serikali katika kutoa elimu ya umoja na amani, kupinga chuki, migawanyiko na vitendo vyovyote vinavyoweza kuvuruga mshikamano wa Taifa.

Amesema kuwa vita yoyote inayohusisha wenyewe kwa wenyewe huwa haina mshindi bali ina kupoteza wote na mgawanyiko ndani ya taifa hauna mshindi bali una matokeo ya kushindwa wote kama Taifa.

Ametoa wito huo (Alhamisi, Desemba 25, 2026) aliposhiriki ibada ya Sikukuu ya Krismasi iliyofanyika katika Kanisa Kuu la Kiinjili la Kilutheri la Azani Front jijini Dar es Salaam.

"Manufaa ya amani ni makubwa: huleta maendeleo ya kiuchumi, huimarisha ustawi wa jamii, na huwezesha kila Mtanzania kushiriki kikamilifu katika kujenga Taifa."

Amesema kuwa Serikali inaendelea kutekeleza wajibu wake wakulinda amani na usalama wa nchi pamoja na kuwajenga Watanzania na hususani vijana kuthamini dhana ya uzalendo kwa nchi yetu.

"Tanzania imeendelea kuwa kielelezo cha umoja, amani, mshikamano na utulivu katika ukanda wetu na barani Afrika. Amani hii imejengwa juu ya misingi imara ya maadili, haki, kuheshimiana, uvumilivu na uzalendo."

Kadhalika, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu ametoa wito kwa wazazi na walezi kuendelea kushirikiana kwa karibu na taasisi za elimu na dini katika kuimarisha malezi ya watoto na vijana kwa kuwajengea misingi imara ya maadili na kuwaongoza kutumia vyema fursa za elimu, teknolojia na utandawazi kwa maendeleo yao na Taifa kwa ujumla.

Aidha, katika Ibada hiyo, Mheshimiwa Dkt. Nchemba ameungana na Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwatakia Wakristo na Watanzania wote kwa ujumla, Heri ya Sikukuu ya Krismasi na kuwasishi kusherehekea kwa Amani, Upendo na Utulivu, kudumisha mshikamano wa Kitaifa kwa maslahi ya Taifa la Tanzania.

Kwa upande wake, Mkuu wa Kanisa la Kiinjili na Kilutheri Tanzania (KKKT) na Mkuu wa Dayosisi ya Mashariki na Pwani, Askofu Dkt. Alex Malasusa amekemea tabia za baadhi ya watu za kuchafua taswira za watu wengine, pamoja na kuichonganisha jamii. Kuna watu wakiona jamii imekaa pamoja kwa amani wao inawakosesha raha".









# DKT. MWIGULU: AMANI HAICHEZEWI.



**WAZIRI MKUU,** Dkt. Mwigulu Nchemba amewataka Watanzania wote kuendelea kuwa makini na kujiepusha na watu wenye nia ovu dhidi ya Tanzania ambao wamekuwa wakihamasisha vurugu ili kuvuruga amani na kuathiri shughuli za kiuchumi na kijamii.

Waziri Mkuu Mwigulu ametoa rai alipozungumza na wakazi wa Kiwira mkoani Mbeya akiwa kwenye ziara ya kikazi ya kukagua miundombinu ya umma na mali za watu binafsi ambazo zimeathirika na vurugu zilizotokea Oktoba 29, 2025.

"Tunaelewa lengo lao ni rasilimali zetu, Tanzania ina rasilimali adhimu barani Afrika na wanajua ili kuzipata ni lazima kuwavuruga Watanzania, hili jambo msikubali, amani yetu ndio kila kitu. Tunapaswa kuendelea kushirikiana kulinda amani."

Mheshimiwa Dkt. Mwigulu ameendelea kusisitiza kwamba pahali ambapo hapana amani hakuna shughuli yoyote ya maeneleo ambayo inaweza kufanyika, hivyo amewahimiza wananchi hususan vijana kuwa makini na kutokubali kutumika.

hivyo amewahimiza wananchi hususan vijana kuwa makini na kutokubali kutumika.

Wakati huo huo, Waziri Mkuu amesisitiza watumishi wa umma kuendelea kuwahudumia wananchi ipasavyo ikiwa ni pamoja na kuwafuata katika maeneo yao, hususani ya pembezoni ili kuwasikiliza na kushirikiana nao kutatua changamoto zao.

Pia, Waziri Mkuu amewataka watendaji wa sekta ya afya kuhakikisha vituo vya kutolea huduma za afya nchini zinakuwa na dawa za kutosha na wanapoagiza dawa wahakikishe wanafanya tafiti na kuagiza dawa kutokana na mahitaji ya eneo husika.

Kabla ya kuzungumza na wananchi Waziri Mkuu alikagua majengo ya Mamlaka ya Mji Mdogo wa Kyela na majengo ya Ofisi ya Kituo cha Forodha kwa Pamoja-Kasumulu ambayo ni miongoni mwa ofisi za umma zilizoathiriwa na vurugu zilizotokea Oktoba 29, 2025.

"

**Tunaelewa lengo lao ni rasilimali zetu, Tanzania ina rasilimali adhimu barani Afrika na wanajua ili kuzipata ni lazima kuwavuruga Watanzania, hili jambo msikubali, amani yetu ndio kila kitu. Tunapaswa kuendelea kushirikiana kulinda amani.**





# DKT MWIGULU AAGIZA ZIUNDWE TIMU ZA MIKOA ZA WAKAGUZI WA MIRADI

**WAZIRI MKUU** Dkt. Mwigulu Nchemba amemwagiza Waziri wa Nchi (OWM-TAMISEMI) awaandikie barua Wakuu wote wa Mikoa ili waunde timu za ukaguzi wa majengo na miradi kwenye mikoa yao kama njia ya kukabiliana na wakandarasi wanaokiuka makadirio ya gharama za ujenzi (BOQ) wa miradi ya Serikali.

"Yuko Mhandisi ambaye huwa anakagua miradi wakati wa mbio za Mwenge wa Uhuru. Wakuu wa Mikoa wote wawe na timu za vijana wa aina hiyo, ili wasiuziwe mbuzi kwenye gunia. Iwe ni utamaduni wa Serikali kufanya ukaguzi wa aina hiyo," amesema Waziri Mkuu.

Ametoa agizo hilo wakati akizungumza na viongozi na wananchi wa Wilaya za Ruangwa na Nachingwea, mkoani Lindi akiwa katika ziara ya siku tatu

Akizungumza mara baada ya kukagua ujenzi wa ofisi za Halmashauri ya Wilaya ya Nachingwea, Waziri Mkuu amesema kuna baadhi ya miradi ambayo wakandarasi wake hawafuati BOQ. "Unakuta BOQ inataka nondo za mm 16 lakini mkandarasi anaweka za mm 12. Kuna mahali zinatakiwa nondo sita, yeye anaweka nondo nne. Jengo likikamilika, huwezi kuona na kulinganisha makubaliano ya BOQ. Nimeelekeza kila mkoa uwe na timu ya wataalamu wa kukagua miradi ya Serikali."

"Mikoa yote wawe na vitengo hivi na wawe pia na vifaa vya kuchunguza majengo na miradi mingine badala ya kusubiri uchunguzi unaofanywa wakati wa mbio za Mwenge wa Uhuru. Vitengo hivyo kazi yao ya kila siku ni kufuatilia miradi ili kubaini maeneo ambako Serikali imetoa fedha na hazijatumika vizuri ili tuweze kuchukua hatua," amesisitiza.

Mapema, Waziri Mkuu aliweka jiwe la msingi katika mradi wa maji wa Lindi-Ruangwa- Nachingwea uliojengwa kwenye kijiji cha Chimbila A wilayani Ruangwa, mkoani Lindi.

Mradi huo ambao chanzo chake kinatoka mito ya Nyangao na Chilua wilayani Lindi, unatekelezwa na Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) pindi utakapokamilka, utanufaisha vijiji 56 katika Wilaya za Ruangwa (vijiji 34), Wilaya ya Nachingwea (vijiji 21) na Wilaya ya Lindi (Kijiji 1).

Akitoa taarifa ya mradi huo, Mkurugenzi Mtendaji wa RUWASA, Mhandisi Walter Kirita amesema mradi huo unatarajiwa kugharimu sh. bilioni 119 na hadi sasa wameshalipa sh. bilioni 49 ambapo ujenzi wake umefikia asilimia 67 ya utekelezaji.

Mradi huo umeanza kutekelezwa Februari, 2023 na awamu ya kwanza (Lot 1) inatarajiwa kukamilika Juni, 2026. Hata hivyo, Mhandisi Kirita alimweleza Waziri Mkuu kwamba ifikapo Februari, 2026 baadhi ya vijiji vitaanza kupata huduma ya maji.


Akizungumza baada ya kuweka jiwe la msingi, Dkt. Mwigulu alisema ameridhishwa na hatua ya utekelezaji wa mradi ambayo imefikiwa. "Hivi ndivyo Rais Dkt. Samia anataka kuona namna kazi inavyofanyika. Hapa tumeona asilimia ya utekelezaji ni kubwa kuliko fedha zilizotolewa hadi sasa. "

Dkt. Mwigulu ametumia fursa hiyo kumpongeza Waziri Mkuu mstaafu, Kassim M. Majaliwa kwa kuasisi mradi huo na kufuatilia fedha za mradi kila mara.

# BANDARI YA UVUVI-KILWA









## THAMANI YA MRADI

Utekelezaji wa mradi huu utagharimu kiasi cha shilingi bilioni 280 pindi utakapokamilika.

## HATUA YA UTEKELEZAJI

Kufikia Desemba 2025, mradi ulikuwa umefikia asilimia 90.

## UMUHIMU WA KIUCHUMI

Bandari hii itasaidia kuongeza thamani ya mazao ya uvuvi, kuwezesha usafirishaji wa samaki kwa soko la ndani na nje, na kuchangia Pato la Taifa (GDP)

## UWEKEZAJI NA AJIRA

Mradi utavutia uwekezaji katika viwanda vya kusindika samaki na kutengeneza ajira, ikiwa ni sehemu ya ahadi ya kuendeleza miradi ya kimkakati.








# DKT MWIGULU: TUACHE TABIA YA KUZOEA MATATIZO

**WAZIRI MKUU** Dkt. Mwigulu Nchemba amewaonya watendaji na watumishi wa umma waache tabia ya kuzoea matatizo hasa katika sehemu zinazotoa huduma kwa wananchi.

Ametoa onyo wakati akizungumza na wagonjwa na watumishi wa Hospitali ya Wilaya ya Nachingwea mkoani Lindi alipofanya ziara ya kushtukiza ili kujionea hali halisi ya utoaji huduma siku za wikiendi katika hospitali hiyo.

Waziri Mkuu ambaye alikuwa na ratiba ya kukagua ujenzi wa ofisi za Halmashauri ya Wilaya ya Nachingwea, mara baada ya kuwasili wilayani humo akitokea Ruangwa, aliamua kuanzia kwanza hospitalini kisha akaenda kwenye ukaguzi wa jengo hilo.

Akiwa hospitalini hapo, alienda moja kwa moja kwenye chumba cha daktari wa zamu ili apate utaratibu wa kumhudumia mgonjwa pindi anapofika.

Hata hivyo, Waziri Mkuu alikuta wagonjwa wawili nje ya vyumba vya madaktari ambao mmoja wao alikuwa na cheti lakini mwingine hakuwa nacho na alishapita mapokezi bila kuelezwa chochote. Na vyumba vya madaktari havikuwa na wagonjwa, licha ya kuwa madaktari walikuwemo.

"Wekeni utaratibu wa kuwaelekeza wagonjwa waende wapi mara tu wanapofika hospitalini. Hapa si mahali pa kuja kufanya matembezi, mtu akija hapa anahitaji kupewa huduma," alisema wakati akiongea na Mganga Mkuu wa Wilaya hiyo.

# WAZIRI MKUU: WIZARA YA AFYA FUATILIENI UPATIKANAJI WA DAWA MAHSUSI

**WAZIRI MKUU** Dkt. Mwigulu Nchemba ameutaka uongozi wa Wizara ya Afya ufuatilie suala la upatikanaji wa dawa mahsusi hospitalini ili kuondoa dosari ndogondogo zilizopo.

Ametoa wito huo (Jumamosi, Desemba 20, 2025) wakati akizungumza na viongozi wa mkoa wa Lindi na viongozi wa sekta ya afya mara baada ya kupokea taarifa ya ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Lindi inayojengwa katika eneo la Mitwero, nje kidogo ya mji wa Lindi.

“Kitengo chenu cha utafiti kifanye kazi kubaini ni aina gani ya dawa zinahitajika hapa mkoani Lindi. Bohari ya Dawa ifuatilie vizuri na kuleta dawa zinazotakiwa,” amesema wakati akimwagiza Naibu Waziri wa Afya, Dkt. Florence Samizi ambaye alikuwepo katika ziara hiyo.

Amesema usipofanyika utafiti huo, Bohari ya Dawa watajikuta wanapeleka dawa nyingi mahali ambako hazihitajiki. “Unaweza kujikuta unapeleka dawa nyingi za malaria huko Zanzibar wakati wao hilo tatizo hawana kabisa,” amesema.

“Kuna kilio cha dawa mahsusi kukosekana katika hospitali na badala yake wagonjwa wanaambiwa waende kununua kwenye viosk.Takwimu zinaonesha kuna utoshelevu wa dawa wa asilimia 80

Takwimu zinaonesha kuna utoshelevu wa dawa wa asilimia 80 – 90 lakini katika hali halisi, watu wanaambiwa wakanunue dawa nje”, amesema.

Kuhusu upatikanaji wa vifaa tiba, Waziri Mkuu amesema ndani ya miaka minne na nusu, Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ameweza kuweka mashine za CT-Scan katika mikoa yote 26 ya Tanzania Bara ikilinganishw ana mashine mbili zilizokuwepo. “Pia ameweka mashine za MRI katika hospitali zote za kanda ili kurahisisha upatikanaji wa huduma za kibingwa, amesema.

Mapema, akitoa maelezo ya ujenzi mbele ya Waziri Mkuu, Mganga Mfawidhi wa hospitali hiyo, Dkt. Alexander Makala alisema ujenzi wa jengo la wagonjwa wa nje umefikia asilimia 85 na baadhi ya huduma zinatolewa katika hospitali hiyo.

Alisema jengo la mionzi lililogharimu sh. milioni 231 limekamilika na linatoa huduma ambapo mashine ya CT-Scan yenye thamani ya sh. bilioni 1.8 imefungwa na inafanya kazi. “Majengo mengine yaliyokamilika ni la magonjwa ya dharura (EMD) kwa gharama ya sh. milioni 650, wagonjwa mahututi (ICU) kwa gharama ya sh. milioni 560 na nyumba ya watumishi kwa gharama ya sh. milioni 55.”






# DKT. MWIGULU AAGIZA KUFUTWA KAZI WATENDAJI WA TEMESA.

**WAZIRI MKUU,** Dkt. Mwigulu Nchemba ameagiza kufutwa kazi na kufikishwa katika vyombo vya sheria kwa aliyekuwa Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Ufundi na Umeme Tanzania (TEMESA) pamoja na Menejimenti ya wakala huo kutokana na ubadhilifu wa zaidi ya shilingi bilioni 2.5.

Pia, Waziri Mkuu amemuagiza Waziri wa Ujenzi, Abdallah Ulega kufanya uchunguzi wa vivuko vyote ili kubaini vyanzo vya uharibifu kwa sababu kuna taarifa kwamba vivuko hivyo vinaharibiwa kwa makusudi ili wahusika waweze kujipatia fedha kupitia matengenezo.

Amesema uamuzi huo unatokana na matokeo ya tume maalumu iliyoundwa ndani ya kuchunguza tuhuma za matumizi mabaya ya fedha za umma katika wakala huo. "Vyombo husika vichukue hatua kwa wahusika, haya mambo ya kutoheshimu fedha za umma, kutokuwa na huruma na Watanzania lazima yafike mwisho."

Waziri Mkuu ametoa agizo hilo Jumatano, Desemba 24, 2025 akizungumza na viongozi wa mkoa wa Dar es Salaam na wakazi wa Kigamboni akiwa katika ziara ya kukagua hali ya utoaji wa huduma katika kivuko cha Magogoni, Kigamboni jijini Dar es Salaam.

Amesema ubadhilifu uliofanyika ni sawa na watendaji hao kugawana vivuko pamoja na kuiba nauli zinazotolewa na wananchi mambo ambayo yanamkera Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan na amewaagiza wayakomeshe ili wananchi waendelee kupata huduma bora na za uhakika.

Pia, Waziri Mkuu amemuagiza Waziri wa Ujenzi, Abdallah Ulega afanye mawasiliano na wizara ya fedha kuhakikisha fedha za malipo ya utengenezaji wa vivuko zinatolewa kwa wakati ili zoezi la ukarabati liweze kukamilika na vivuko hivyo viweze kutoa huduma. Serikali inavivuko vitatu katika eneo la Kivukoni/Kigamboni na kwa sasa kinachonfanyakazi ni kimoja tu.

Kwa upande wake, Kaimu Mtendaji Mkuu wa TEMESA, Moses Mabamba amesema Serikali inamiliki vivuko vitatu kwa ajili ya Kivukoni na Kigamboni ambapo kwa sasa kinachotoa huduma ni kimoja tu cha MV. Kazi huku kivuko cha MV. Magogoni kipo kwenye matengenezo Mombasa tangu 2023.

Amesema matengenezo hayo ambayo yanagharimu takribani shilingi bilioni 7.5 yamefikia asilimia 70 huku kivuko kingine cha MV. Kigamboni kipo katika matengenezo kwenye kampuni ya Songoro Marine, Kigamboni.

#TANZANIA NI YETU

TUILINDE NA TUITUNZE

Ofisi ya Waziri Mkuu